# SERIKALI MTANDAO

Tuijenge Serikali kidijtali

www.ega.go.tz

Toleo la 14 | Octoba - Disemba 2025

# Mageuzi ya Kidijitali Serikalini yaipaisha Tanzania kimataifa

- Tanzania yatinga Kundi la Juu la Ukomavu wa TEHAMA Duniani kwa mara ya pili.
- Ripoti ya Benki ya Dunia yathibitisha Mafanikio ya Mageuzi ya TEHAMA Serikalini



Wadau wa Serikali Mtandao kukutana Arusha Februari 2026

>>>Uk 08

Mamlaka ya Serikali Mtandao yapata Ithibati ya Kimataifa ya ISO/IEC 27001:2022

>>>Uk 09

Afya : Asilimia kubwa ya wafanyakazi wanakabiliwa na changamoto ya Afya ya akili

>>>Uk 18

Mapinduzi ya Serikali Mtandao - Hamlashauri ya Wilaya ya Geita Mapato yaongezeka kutoka Bilioni 4 hadi Bilioni 18

>>>Uk 20

# Yaliyomo


**Nukuu**

Nukuu kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao **Uk.3**

**Dira yetu**

Kuimarisha ushirikiano na wadau katika kujenga Serikali Mtandao imara **Uk.4**

**Tahariri**

MGOV-Suluhishi la Kidijitali kwa Taasisi za Umma **Uk. 5**

**Habari**

Mageuzi ya Kidijitali yaipaisha Tanzania Kimataifa **Uk. 6-7**

**Habari**

Wadau wa Serikali Mtandao kukutana Arusha Februari 2026 **Uk. 8**

**Habari**

Mamlaka ya Serikali Mtandao yapata ithibati ya kimataifa ya ISO/IEC 27001:2022 **Uk. 9**

**Habari**

Serikali yasisitiza katika uwekezaji wa mafunzo ya Teknolojia kwa watumishi **Uk.10**

**Habari**

Hudumieni Umma kwa kuchapisha taarifa sahihi :e-GA **Uk.11**

**Habari**

Maafisa waandamizi watakiwa kudumisha uadilifu **Uk.12**

**Habari**

e-GA yatambulisha kwa wadau Mfumo wa e-Board toleo la pili **Uk.13**

**Habari**

e-GA yasisitiza umuhimu wa nyaraka zinazotekelezeka katika usimamizi wa TEHAMA Serikalini **Uk.14-15**

**Vijana na TEHAMA**

Safari ya ndoto za Kidijitali za PULCHERIA **Uk. 16-17**

**Afya**

Asilimia kubwa ya wafanyakazi wanakabiliwa na matatizo yanayohusiana na Afya ya akili **Uk. 18**

**Makala**

Mapinduzi ya Serikali Mtandao - Halmashauri ya Wilaya ya Geita **Uk. 20-22**

**Wasemavyo wadau**

**Uk.17-23**

**Matukio katika Picha**

**Uk. 24**



> Serikali Mtandao katika sekta ya elimu ni daraja la maarifa linalounganisha Walimu, Wanafunzi, Wazazi na Serikali kupitia teknolojia. Kupitia mifumo madhubuti ya TEHAMA, Inarahisisha upatikanaji wa rasilimali za kujifunzia, taarifa za kitaaluma na usimamizi wa taasisi za elimu. Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na sekta ya elimu, inaendelea kusimamia kwa makini ujenzi wa miundombinu ya kidijitali itakayowezesha elimu bora, jumuishi na endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

**Dkt. Mussa Kissaka**
**Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi**



Mhandisi Benedict Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

# Kuimarisha Ushirikiano na Wadau Katika Ujenzi wa Serikali Mtandao Imara

Katika safari ya kuijenga Tanzania ya kidijitali, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) inaamini kuwa ushirikiano wa karibu na wadau wa Serikali Mtandao ndiyo nguzo kuu ya mafanikio ya mageuzi ya matumizi ya TEHAMA Serikalini.

Dira yetu ni kuimarisha na kuendeleza ushirikiano thabiti kati ya e-GA na wadau wake wote, wakiwemo taasisi za umma, sekta binafsi, wadau wa maendeleo, wataalamu wa TEHAMA na wananchi, ili kujenga Serikali Mtandao iliyo jumuishi, salama na yenye ufanisi katika utoaji wa huduma.

Katika kutekeleza dira hii, e-GA inaendelea kuratibu na kusimamia matumizi ya TEHAMA serikalini kwa kuhakikisha uwepo wa mifumo ya pamoja ya Serikali, kuimarisha muunganiko wa mifumo (interoperability) ya taasisi mbalimbali, pamoja na kuweka sera, viwango na miongozo vinavyochochea matumizi bora ya TEHAMA kwa maslahi ya umma.

Vilevile, e-GA inajidhatiti kushirikisha wadau wake katika hatua zote za kubuni, kuendeleza, kuboresha na kusimamia mifumo ya Serikali Mtandao, kutoa mafunzo na kujenga uwezo kwa watumiaji, sambamba na kuhimiza utamaduni wa kupokea mrejesho ili mifumo ya kidijitali iendelee kukidhi mahitaji halisi ya Serikali na wananchi.

Ushirikiano huu ni muhimu katika kuhakikisha huduma za Serikali zinaunganishwa, zinapatikana kwa urahisi na haraka, zinaendeshwa kwa uwazi na zinazingatia misingi ya uwajibikaji. Aidha, unasaidia kupunguza gharama za uendeshaji, kuongeza ufanisi wa maamuzi na kuimarisha usalama wa mifumo ya TEHAMA na taarifa za Serikali.

Kupitia dira hii, e-GA inalenga kujenga ikolojia imara ya Serikali Mtandao inayochochea ubunifu wa kiteknolojia, kukuza matumizi salama ya TEHAMA na kuimarisha uchumi wa kidijitali, hatimaye kufanikisha azma ya Serikali ya kidijitali inayomlenga mwananchi na kuleta maendeleo endelevu ya taifa.

Tunawahimiza wadau wote kushirikiana nasi katika safari ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Ushirikiano wenu ni muhimu ili kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inawasaidia wananchi, kurahisisha huduma na kukuza maendeleo ya kidijitali nchini.

Katika kuimarisha ushirikiano wetu nitumie fursa hii kuwakaribisha wadau wote wa Serikali Mtandao katika Mkutano wa 6 wa Serikali Mtandao utakaofanyika Februari **17 – 19 jijini Arusha.**

Kaulimbiu yetu ya mwaka huu ni "Kuboresha Utendaji wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma Kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao"(**"Transforming government operations by enhancing public service delivery through integrated and secure government solutions").**



Bi. Subira Kaswaga
Meneja Mawasiliano

# mGOV – Suluhisho la Kidijitali kwa Taasisi za Umma

Katika zama za sasa, teknolojia ya kidijitali imechukua nafasi muhimu katika utoaji wa huduma za umma. Moja ya suluhisho bunifu lililofanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ni ujenzi wa Mfumo wa Huduma za Serikali kwa Simu za Mkononi (mGov).

Mfumo huu unawezesha taasisi za umma kutoa huduma kwa haraka, kwa uwazi, na kwa urahisi zaidi kupitia teknolojia za mawasiliano ya simu na vifaa vya mkononi.

Aidha, mfumo huu unarahisisha taratibu kama vile usajili wa huduma, malipo ya kodi na ada, kwa kutumia simu au kompyuta, na kupata taarifa muhimu kwa wakati halisi. Faida zake kwa taasisi ni kama vile kupunguza urasimu, kuongeza uwazi, kupunguza matumizi ya rasilimali wat una fedha, kuongeza ubora wa utoaji wa huduma za umma na kuboresha usimamizi wa taarifa.

Kwa upande wa wananchi, mGov hurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa wakati wowote na mahali popote kupitia teknolojia za mawasiliano ya simu na vifaa vya mkononi. Aidha, humpunguzia mwananchi gharama na muda wa ufuatiliaji wa huduma mbalimbali za serikali, kwani nyingi hutolewa kwa njia za ujumbe mfupi (SMS) au kupitia namba ya msimbo (USSD) ya *152*00# Njia hizi hazihitaji mtandao wa intaneti au simu janja, hivyo kuwafikia wananchi waishio mijini na vijijini kwa urahisi zaidi na kwa gharama nafuu.

Hata hivyo, pamoja na faida hizi, bado baadhi ya taasisi hazijaanza kutumia mfumo huu, jambo linalosababisha ucheleweshaji wa huduma, kuongeza gharama zisizo za lazima au kushindwa kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa haraka.

Ni wakati muafaka kwa taasisi za umma kutumia mfumo wa mGov. Kutumia mfumo huu sio tu kuboresha huduma za umma, bali pia inasaidia kuimarisha uwazi na uwajibikaji.

Tunawahimiza viongozi wa taasisi za umma kutambua faida hizi na kuchukua hatua za haraka za kujiunga na mfumo wa mGov. Dunia ya kidijitali inakimbia kwa kasi kubwa, na taasisi yoyote kubaki nyuma katika utoaji wa huduma zake kupitia simu za kiganjani inamaanisha kuiacha jamii nyuma. Jiunge na mGov leo, na uwe sehemu ya utumishi bora wa umma!




## BODI YA UHARIRI

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti | Eng. Benedict B. Ndomba<br>Mkurugenzi Mkuu |
| Mhariri | Subira J. Kaswaga<br>Meneja Mawasiliano |
| Wajumbe | Erick Kalembo<br>Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji<br>SACP. Hamis Ali<br>Mkaguzi mkuu wa Ndani<br>SACP. Rafael Ruthahiwa<br>Meneja wa Huduma za Sheria<br>Long'ida Oltetiai<br>Meneja wa Huduma kwa wateja na Takwimu |



# Mageuzi ya Kidijitali Serikalini yaipaisha Tanzania Kimataifa

- **Tanzania yatinga Kundi la Juu la Ukomavu wa TEHAMA Duniani kwa mara ya pili.**
- **Ripoti ya Benki ya Dunia yathibitisha Mafanikio ya Mageuzi ya TEHAMA Serikalini**

Na. Benchine Bago | Afisa Habari

Tanzania imeendelea kung'ara kimataifa baada ya Benki ya Dunia (World Bank - WB) kuitaja kuwa miongoni mwa nchi zilizo na ukomavu wa juu wa matumizi ya TEHAMA katika sekta ya umma, hatua inayothibitisha mafanikio ya mageuzi ya kidijitali yanayoendelea kutekelezwa na Serikali.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Ukomavu wa Matumizi ya Teknolojia Duniani katika Utoaji wa Huduma za Serikali na Ushirikishwaji wa Wananchi 'GovTech Maturity Index - GTMI' ya Benki ya Dunia mwaka 2025, Tanzania imeorodheshwa katika Kundi A - Ukomavu wa Juu wa matumizi ya TEHAMA (Extensive GovTech Maturity), kundi linalojumuisha nchi zinazoongoza duniani katika matumizi ya teknolojia katika kuboresha utoaji wa huduma za serikali na ushirikishwaji wa wananchi.

Ripoti hiyo hutathmini kiwango cha ukomavu wa matumizi ya TEHAMA serikalini takriban katika nchi zote duniani, kwa kuzingatia maeneo mbalimbali yakiwemo sera, sheria, miongozo, mifumo na utekelezaji wake, ambapo katika mwaka uliopita ripoti hiyo ilitolewa mwezi Desemba, 2025.

Hii ni mara ya pili kwa Tanzania kutambuliwa na Benki ya Dunia (WB) katika kupiga hatua ya ukomavu wa TEHAMA, ambapo mwaka 2022 Tanzania ilitajwa kuwa miongoni mwa nchi zilizofanya vizuri zaidi duniani katika GovTech Maturity Index. Katika utafiti huo uliohusisha nchi 198, Tanzania ilipanda kutoka nafasi ya 90 mwaka 2021 hadi nafasi ya 26 mwaka 2022 na kutoka kundi B hadi kundi A. Barani Afrika, Tanzania ilishika nafasi ya pili baada ya Mauritius na kuwa kinara wa ukanda wa Afrika Mashariki.

## Kuimarika kwa Nafasi ya Tanzania Kimataifa

Mafanikio haya ni mwendelezo wa safari ya Tanzania ya kupanda ngazi katika ukomavu wa matumizi ya TEHAMA Serikalini, na kuendelea kujijengea taswira chanya kikanda na kimataifa. Tanzania imeendelea kuonesha uthabiti katika matumizi ya teknolojia kama nyenzo wezeshi ya kuboresha ufanisi katika taasisi za umma, kuongeza uwazi na kuimarisha uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa upande wa bara la Afrika, Tanzania imeendelea kuwa miongoni mwa nchi vinara wa mageuzi ya kidijitali Serikalini, ikilinganishwa na mataifa mengine yaliyofanyiwa tathmini katika ripoti hiyo. Tanzania ni moja kati ya nchi tano tu katika bara la Afrika, ambazo zimeingia kwenye kundi la juu la ukomavu wa TEHAMA Serikalini, nchi nyingine ni Kenya, Misri, Uganda na Rwanda.

Ripoti ya GovTech Maturity Index (GTMI) 2025 imeangazia maeneo makuu manne ya TEHAMA:

i. Mifumo Mikuu ya Serikali (Core Government Systems)
iii. Huduma Zinazotolewa Mtandaoni (Online Public Service Delivery)
v. Jukwaa la Ushirikishwaji Wananchi Kidijitali (Digital Citizen Engagement)
vii. Mazingira Wezeshi (GovTech Enablers).

## Mifumo ya Mikuu ya Serikali yachochea Mafanikio

Ripoti ya Benki ya Dunia inaonesha kuwa, mafanikio ya Tanzania yametokana kwa kiasi kikubwa na uwepo na matumizi ya Mifumo ya Mikuu ya Serikali (Core Government Systems). Mifumo hiyo imejumuisha mifumo ya usimamizi wa rasilimaliwatu kama vile Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Mishahara (Human Capital Information Management System - HCIMS), Mfumo wa Ajira katika Utumishi wa Umma (Ajira Portal), pamoja na mifumo ya kuunganisha na kubadilishana taarifa kati ya taasisi za umma (interoperability).

## Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus–GovESB)

umetajwa kuwa mhimili muhimu unaowezesha mifumo ya taasisi mbalimbali za umma kusomana na kubadilishana taarifa kwa usalama na ufanisi zaidi. Hatua hii imepunguza urudufu wa taarifa, kuharakisha utoaji wa huduma na kuongeza uwajibikaji.

## Ushirikishwaji wa Wananchi Kidijitali

Katika eneo la Ushirikishwaji wa Wananchi Kidijitali (Digital Citizen Engagement), Tanzania imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazochukua hatua madhubuti katika kujenga mifumo inayowawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika masuala ya utawala.



Mhandisi Benedict Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Mfumo wa e-Mrejesho umekuwa ni nyenzo muhimu inayowaunganisha wananchi na Serikali, kwa kuwezesha utoaji wa maoni, malalamiko, ushauri na pongezi, pamoja na kupata mrejesho kwa wakati. Mfumo huu umechangia kuimarisha uwazi, uwajibikaji na imani ya wananchi kwa Serikali.

## Mazingira Wezeshi (GovTech Enablers)

Ripoti hiyo pia inaonesha kuwa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao (GovTech Enablers) vimekuwa chachu ya mafanikio ya Tanzania katika mageuzi ya kidijitali. Mazingira haya rafiki yameiwezesha Serikali kuwekeza na kusimamia miradi ya TEHAMA kwa mweleke mmoja wa kitaifa.

## Utoaji wa Huduma Mtandaoni (Online Public Service Delivery)

Aidha, utoaji wa huduma za serikali kwa njia ya mtandao (Public Service Delivery) kupitia mifumo mbalimbali ikiwemo Mfumo Mkuu wa Malipo Serikalini (GePG), Mfumo wa Kitaifa wa Manunuzi ya Kielektroniki (NeST) na mifumo ya huduma za Serikali za Mitaa (TAUSI), umeongeza upatikanaji wa huduma kwa wananchi kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

## Mtazamo wa e-GA

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba, amesema kuwa mafanikio hayo ni ushahidi wa mwelekeo sahihi wa taifa katika kujenga Serikali ya kidijitali.

> **“World Bank imefanya utafiti huu kwa takriban mwaka mmoja huku ikikusanya uthibitisho na taarifa mbalimbali kwenye matumizi ya TEHAMA Serikalini (Evidence-based GovTech Maturity Index Survey) katika nchi mbalimbali duniani.”**
>
> Mhandisi Benedict Ndomba.
> **Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Amesisitiza kuwa, uwepo wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA serikalini unaonesha usimamizi mzuri wa rasilimali za TEHAMA, na kutoa wito kwa taasisi za umma kuendelea kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA. Pia amehimiza matumizi ya mifumo ya ushirikishwaji wa wananchi na kuunganisha mifumo ya taasisi na GovESB.

Mafanikio haya yanaifanya Tanzania kuwa kielelezo cha mageuzi ya kidijitali barani Afrika, na kuweka msingi imara wa kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za umma, kukuza uwazi na kuimarisha uchumi wa kidijitali kwa maendeleo endelevu ya taifa.



# Wadau wa Serikali Mtandao Kukutana Arusha Februari 2026

Na. Benchine Bago | Afisa Habari

Wadau wa Serikali Mtandao kutoka katika sekta mbalimbali ndani na nje ya nchi, wanatarajia kukutana jijini Arusha mapema mwezi Februari mwaka 2026 katika Mkutano wa Sita wa Serikali Mtandao.

Takribani wadau zaidi ya 1000 kutoka katika taasisi na mashirika mbalimbali ya umma nchini, pamoja na wageni kutoka nje ya Tanzania, wanatarajiwa kukutana katika mkutano huo utakaofanyika tarehe 17 hadi19 Februari, 2026, katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC), jijini Arusha.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba amesema, mkutano huo ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka katika kuratibu, kusimamia, kuendeleza na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini, sambamba na kuimarisha ushirikiano baina ya e-GA na wadau wake.

> **"Hili ni jukwaa muhimu linalowakutanisha wataalamu, viongozi na watumiaji wakuu wa mifumo ya Serikali Mtandao ili kujadili mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo, na namna bora ya kuimarisha zaidi utoaji wa huduma za umma kwa njia ya TEHAMA".**
>
> Mhandisi Benedict Ndomba
> **Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Ndomba amebainisha kuwa, Mgeni rasmi wa mkutano huo anatarajiwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi Ndg. Balozi Moses Kusiluka. Aidha, mkutano utaongozwa na kaulimbiu isemayo: "Kuboresha Utendaji wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma Kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao."

Kaulimbiu hiyo inasadifu uelekeo wa Serikali katika kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA inayojengwa serikalini, inakuwa Madhubuti na salama ili iweze kutumika kwa usahihi na kuleta tija kwa wananchi, kuongeza uwajibikaji, usalama wa taarifa, na kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za umma.

Mhandisi Ndomba amewataka wadau wote wa serikali mtandao wakiwemo Maafisa Masuuli, Wakurugenzi, Wakuu wa TEHAMA, Maafisa Mawasiliano, Mipango, Fedha, Rasilimali Watu, Manunuzi, Watunza Kumbukumbu, pamoja na Watumiaji wote wa mifumo ya TEHAMA serikalini, kushiriki kikamilifu katika mkutano huo.

"Uwepo wa makundi haya ni chachu katika kukuza jitihada za Serikali Mtandao, kwa sababu wao ndio watumiaji wakuu wa mifumo, hivyo majadiliano yatakayofanyika katika mkutano huo yatasaidia kuongeza uelewa wa pamoja na kuimarisha utendaji katika taasisi zao." amefafanua Mhandisi Ndomba.

Kwa upande wake Meneja wa Mawasiliano wa e-GA, Bi. Subira Kaswaga, ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya Maandalizi ya mkutano huo, amethibitisha kuwa, taratibu zote muhimu zinaendelea vizuri, ikiwa ni pamoja na maandalizi ya ukumbi, ratiba pamoja na kutoa msaada wa kiufundi kwa washiriki wanaoendelea kujisajili kupitia Mfumo wa TSMS.

# Mamlaka ya Serikali Mtandao yapata Ithibati ya Kimataifa ya ISO/IEC 27001:2022

Na. Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA,) imepata Ithibati ya Kimataifa ya ISO/ IEC 27001:2022, baada ya mifumo na taratibu zake za usimamizi wa usalama wa taarifa kutambuliwa na kukidhi viwango vya juu vya kimataifa.

Ithibati hii inaonesha dhamira ya Mamlaka katika kulinda taarifa za Serikali na kuhakikisha utoaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa usalama, ubora na uaminifu, ikiwa ni hatua muhimu katika kuboresha huduma za Serikali zitolewazo kwa njia ya kidijitali.

Kupitia utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Usalama wa Taarifa (ISMS) Mamlaka imeimarisha ulinzi wa taarifa na kuongeza uthabiti wa mifumo kwa kusimamia vihatarishi vya TEHAMA kwa ufanisi zaidi, sambamba na matakwa ya viwango vya ISO/IEC 27001:2022.

Akizungumza katika mahojiano maalumu jijini Dodoma, Meneja wa Kitengo cha Usimamizi wa Vihatarishi na Ubora wa TEHAMA wa e-GA Bi. Farida Juma, anasema kadiri wananchi wanavyoendelea kutegemea mifumo ya kidijitali kupata huduma za Serikali, umuhimu wa kulinda usalama wa taarifa na mifumo umezidi kuwa mkubwa.

Kwa kutambua ongezeko la mahitaji ya huduma salama, thabiti na zinazotegemewa za Serikali mtandao, Mamlaka ilianzisha juhudi mahsusi za kuimarisha usalama wa taarifa kupitia utekelezaji wa ISMS na kupata cheti cha **Ithibati cha ISO/IEC 27001:2022.**

Alisema, kupitia ISMS Mamlaka imefanikiwa kuimarisha ulinzi na usimamizi wa taarifa za Serikali, kuongeza uwajibikaji kwa watumishi na kukuza uelewa wa masuala ya usalama wa taarifa sambamba na kupunguza vihatarishi vinavyoweza kuathiri utoaji wa huduma.

Aidha, aliongeza kuwa ongezeko la mashambulizi ya kimtandao duniani limeifanya e-GA kuongeza juhudi na kutumia mifumo bora ya usalama, ambapo ISMS imeongeza uwezo wa Mamlaka kukabiliana na vitisho vya kisasa vya kimtandao na kulinda taarifa nyeti za Serikali.

Bi. Farida alisisitiza kuwa, ithibati hii ya **ISO/IEC 27001:2022** inaonesha mtazamo wa kimkakati na wenye mwelekeo wa kujenga mifumo, thabiti na yenye kuaminika na hivyo kuwa mfano wa kuigwa kwa taasisi nyingine nchini katika kuimarisha usalama wa taarifa kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla.



**Bi. Farida Juma**
Meneja wa Kitengo cha Usimamizi wa Vihatarishi na Ubora wa TEHAMA wa e-GA

**"Wajibu wetu kama Mamlaka ya Serikali Mtandao ni kulinda taarifa za Serikali, hivyo ithibati hii ya Kimataifa ni hatua muhimu katika kujenga uaminifu kwa wadau na kuhakikisha huduma za Serikali zinapatikana kwa usalama na ufanisi zaidi"**

Bi. Farida Juma
Meneja wa Kitengo cha Usimamizi wa Vihatarishi na Ubora wa TEHAMA wa e-GA



# Serikali yasisitiza Uwekezaji Katika Mafunzo ya Teknolojia kwa Watumishi

Na. Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), ameitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kuwajengea uwezo watumishi wake katika matumizi ya teknolojia mpya zinazoibukia (Emerging Technologies), ili kuhakikisha zinatumika kwa usalama na kuleta tija inayokusudia.

Mhe. Ridhiwani ametoa rai hiyo Novemba 25 Mwaka 2025, alipozungumza na watumishi wa e-GA wakati alipofanya ziara ya kikazi katika Ofisi za Mamlaka jijini Dodoma.

Alisema kuwa, teknolojia hukua na kubadilika kila mara hivyo, ni muhimu kwa e-GA kuhakikisha watumishi wake wanapata mafunzo mbalimbali kuhusu teknolojia hizo na kuangalia namna zinavyoweza kutumika na kuleta tija kwa taifa.

“Kasi ya ukuaji wa teknolojia duniani imeleta mwelekeo mpya katika uongozi na utendaji kazi, sambamba na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za Serikali, lakini ili tuweze kutumia teknolojia hizi ni lazima tuwekeze katika kuwajengea uwezo watumishi wetu ili waweze kuangalia namna Tanzania inavyoweza kuzitumia na kunufaika nazo”, alisisitiza Mhe. Ridhiwani.

Aidha, aliongeza kuwa teknolojia ni eneo muhimu ambalo likitumika vizuri litasaidia kupunguza changamoto ya ajira nchini, kwani vijana wengi wanaweza kujiajiri kupitia matumizi ya teknolojia mbalimbali na hivyo kujikwamua kiuchumi.

Alisema, pamoja na matumizi ya teknolojia kuongezeka kwa kasi duniani ni muhimu kama taifa liwe na uratibu mzuri wa teknolojia hizo, ili kuhakikisha zinatumika kwa manufaa na kuleta tija iliyokusudiwa.

“Kadri kasi ya matumizi ya teknolojia yanavyoongezeka hatari za kiusalama nazo zinaongezeka, hivyo e-GA mnao wajibu mkubwa wa kuhakikisha mnaimarisha usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini dhidi ya matishio ya usalama wa kimtandao”, aliongeza Mhe. Ridhiwani.

Sambamba na hilo, Mhe. Ridhiwani alipongeza e-GA kwa kuendelea kuimarisha usalama wa mifumo, na kusisitiza umuhimu wa kuwajengea uwezo watumishi katika usalama wa kimtandao ili kuweza kukabiliana na uhalifu wa kimtandao kadiri teknolojia inavyokua.

Kwa upande wake Naibu Waziri Mhe. Regina Ndege, aliwashukuru watumishi wa e-GA kwa mapokezi mazuri na kuwasihi kuimarisha ushirikiano na Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake, ili kuiwezesha Serikali kufikia malengo ya kuwa na Serikali Mtandao yenye tija.

Aliongeza kuwa, Serikali ya awamu ya sita imejidhatiti katika kuimarisha matumizi ya Serikali Mtandao na kuwa Wizara kupitia e-GA, imepewa jukumu hilo muhimu la kuhakikisha inafikia malengo hayo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba, aliahidi kuendelea kutoa ushirikiano na Wizara sambamba na kutekeleza kwa wakati maelekezo yote yatakayotolewa ili kujenga Serikali Mtandao yenye tija.

Hii ni ziara ya kwanza ya kikazi kwa viongozi hao wa Wizara, tangu kuteuliwa kwao na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba mwaka 2025.

# Hudumieni Umma kwa Kuchapisha Taarifa Sahihi : e-GA

Na. Catherine Peter | Afisa Habari Mwandamizi



Bw. Erick Kalembo
Mkurugenzi wa Huduma za Uwezeshaji e-GA

Maafisa Habari Serikalini, wametakiwa kuzingatia weledi katika uandaaji na utoaji wa taarifa za Serikali kupitia tovuti za taasisi, ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu shughuli na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali kupitia tovuti hizo.

Wito huo umetolewa Novemba a 2025, na Mkurugenzi wa Huduma za Uwezeshaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Bw. Erick Kalembo, wakati akifungua mafunzo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Tovuti za Serikali, kwa Wakuu wa Vitengo vya Habari na Mawasiliano Serikalini, pamoja na Maafisa Habari wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya.

Bw. Kalembo alisema kuwa, sekta ya afya imebeba uhai wa wananchi na hivyo ni muhimu kwa Maafisa Habari kuhakikisha wanahuisha na kuweka taarifa sahihi kwenye tovuti, ili kuwawezesha wananchi kupata taarifa na elimu muhimu kuhusu masuala mbalimbali ya afya, pamoja na kufahamu jitihada zinazofanywa na Serikali, katika kuimarisha sekta ya afya.

“Maafisa Habari mmepewa dhamana kubwa ya kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi zinazohusu Serikali, ikiwemo miradi ya maendeleo, lakini ninyi mliopo sekta ya afya mnayo dhama kubwa zaidi ya kulinda na kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala ya afya ikiwemo magonjwa ya milipuko kwa kuweka taarifa sahihi katika tovuti”, alisema Kalembo.

Aliongeza kuwa, jukumu la Maafisa Habari ni pamoja na kufanya uchambuzi yakinifu wa taarifa kwa kuzingatia misingi na weledi wa uandishi wa habari, kabla ya kuziweka kwenye tovuti kwa maslahi mapana ya taifa.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa wataalamu hao kuwasiliana na e-GA mara wanapokutana na changamoto zozote za kiufundi katika upandishaji wa taarifa kwenye tovuti wanazozisimamia, ili kupata ufumbuzi na kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata taarifa sahihi kwa wakati.

“Kwa kuzingatia kasi ya mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, ni muhimu kuboresha tovuti zenu mara kwa mara kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo mbalimbali inayosimamia tovuti za Serikali, ukiwemo Mwongozo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Tovuti za Serikali wa mwaka 2014 na Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama wa Vifaa, Data na Mifumo ya TEHAMA Serikalini wa mwaka 2022”, alisisitiza Bw. Kalembo.

Kwa upande wake, Bi. Rozina Suka, Afisa Habari Mwandamizi wa Hospitali ya Tumbi na mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, ameipongeza e-GA kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yalilenga kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuendesha tovuti za Serikali, pamoja na kuwapatia uelewa kuhusu Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019.

Katika mafunzo hayo, mada mbalimbali ziliwasilishwa zikiwa na lengo la kuongeza uwezo wa Maafisa Habari katika usimamizi wa maudhui na kuimarisha weledi katika utoaji wa taarifa kupitia tovuti pamoja na nafasi ya Maafisa Habari katika kuimarisha na kujenga Serikali Mtandao.

Mada hizo zilijumuisha Sheria ya Serikali Mtandao, matumizi ya teknolojia zinazoibukia, usalama wa tovuti, na usimamizi wa mitandao ya kijamii ili kuwawezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimtandao. Mafunzo hayo ya siku nne yalifanyika kuanzia Novemba 18 hadi 21, mwaka 2025 mkoani Morogoro. Mafunzo hayo ni mkakati wa e-GA wa kuwajengea uwezo Maafisa Habari Serikalini katika kuimarisha utoaji wa taarifa za Serikali kupitia tovuti.




Mhandisi Benedict Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

# Maafisa Waandamizi Watakiwa Kudumisha Uadilifu

Na. Catherine Peter | Afisa Habari Mwandamizi

Maafisa waandamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wametakiwa kuimarisha uadilifu na kuzingatia vipaumbele vya taasisi na Serikali, ili waweze kuwa viongozi bora wa sasa na baadaye.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya uongozi yaliyofanyika hivi mkoani Morogoro.

Ndomba alisema, mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo Maafisa wakuu na waandamizi wa Mamlaka, ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu yao, sambamba na kuongeza mchango katika kuleta mabadiliko chanya ndani ya taasisi.

> **“Mafunzo haya ni mojawapo ya juhudi endelevu za serikali, ili kuhakikisha Maafisa wakuu na waandamizi wanakuwa chachu ya mabadiliko katika taasisi, kwani wao ndio viongozi wa baadaye wa taifa hili.”**
>
> Mhandisi Benedict Ndomba.
>
> **Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Aidha, alieleza kuwa mafunzo hayo yatawasaidia washiriki kusimamia rasilimali watu kwa weledi, kuwa mfano wa kuigwa, na kuboresha utendaji wao wa kila siku. Alisisitiza kuwa uadilifu na weledi ni misingi isiyoweza kupuuzwa katika uongozi wowote unaotaka kufanikiwa.

Ndomba aliongeza kuwa, Mamlaka inatarajia kuona washiriki hao wakiwa na maarifa na mbinu za kisasa zaidi zitakazoongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu yao, ikiwa ni pamoja na kuwa viongozi wazuri kwa Maafisa walio chini yao mara tu baada ya kumaliza mafunzo hayo.


Kwa upande wake, mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Bi. Jackline Jackson, ameishukuru Mamlaka kwa kuandaa mafunzo hayo akisema yatawasaidia kuwaongezea uwezo wa kufanya maamuzi sahihi, kuongoza watu na kuongeza ufanisi wa utendaji katika taasisi.

“Mafunzo haya yatatusaidia kuongoza kwa kuzingatia kanuni, misingi ya maadili, uwajibikaji, haki na kufanya maamuzi ya kimkakati yenye manufaa kwa taasisi,” alisema Bi. Jackline.

Mafunzo hayo ya siku mbili, yalifanyika kuanzia Novemba 13 hadi 14 Mwaka 2025 mjini Morogoro, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mamlaka unaolenga kuwaandaa Maafisa wakuu na waandamizi kuwa viongozi wa baadaye.

# e-GA yawatambulisha wadau Toleo Jipya la Mfumo wa e-BOARD

- **Maboresho yalenga ufanisi wa vikao vya bodi na menejimenti**




Na. Mussa Enock | Afisa Habari

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imewatambulisha watumiaji na wadau wa Mfumo wa Uendeshaji wa Vikao vya Bodi na Menejimenti kwa njia ya mtandao (e-Board) toleo la pili (e-Board V2), likiwa na maboresho yanayolenga kuongeza ufanisi, kurahisisha utoaji wa maamuzi na kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao katika taasisi za umma.

Akifungua kikao kazi kilichoandaliwa na e-GA kwa ajili ya kuwapitisha watumiaji wa mfumo huo kilichofanyika Novemba 28, 2025 jijini Dodoma, Meneja wa Huduma za Sheria wa e-GA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi (SACP) Rafael Rutaihwa, amezisihi taasisi za umma kuimarisha matumizi ya mfumo wa e-Board kama njia ya kisasa ya kuendesha vikao vya bodi, menejimenti pamoja na mabaraza ya madiwani.

Rutaihwa amesema matumizi ya mfumo huo yataisaidia Serikali kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao, hususan matumizi makubwa ya karatasi na gharama za uchapaji sambamba na kuokoa muda.

"Nazisihi Taasisi za Umma kutumia mfumo huu kwani utasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao. Sote tunafahamu idadi ya karatasi zinazotumika katika maandalizi ya vikao pamoja na gharama za uchapaji, ambazo ni kubwa ukilinganisha na matumizi ya mfumo huu," amesema Rutaihwa.

Ameongeza kuwa, pamoja na kupunguza gharama, mfumo wa e-Board unachangia kulinda mazingira kwa kupunguza ukataji wa miti inayotumika kutengenezea karatasi, sambamba na kuongeza ufanisi na urahisi wa viongozi kutoa maamuzi kupitia mifumo ya kidijitali iliyo salama na inayorahisisha upatikanaji wa taarifa.

Kwa upande wake, Afisa TEHAMA wa e-GA, Bw. Juvenali Tarimo, amesema toleo la pili la mfumo wa e-Board limeboreshwa kwa kuzingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa na watumiaji wa toleo la awali la mfumo huo.

"Baada ya kutengeneza mfumo wa e-Board, tulipokea maoni mbalimbali kutoka kwa watumiaji wa toleo la kwanza, maoni hayo yamezingatiwa na kufanyiwa kazi. Lengo la kikao kazi hiki ni kutambulisha toleo jipya la mfumo, kueleza maboresho na vipengele vipya vilivyoongezwa, pamoja na kuwapa watumiaji fursa ya kuhakiki mahitaji ya mfumo na kutoa maoni kabla ya uzinduzi rasmi," amesema Tarimo.

Mfumo wa e-Board unalenga kuboresha uratibu wa vikao vya ngazi mbalimbali, ikiwemo vikao vya Bodi, Madiwani, Kamati na Menejimenti za Taasisi za Umma, huku ukipunguza gharama za uendeshaji na matumizi ya karatasi katika utendaji kazi wa Serikali.

Matumizi ya mfumo huo ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, kifungu cha 29(1), kinachoelekeza Taasisi za Umma kutumia mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuongeza ufanisi na uwazi katika utoaji wa huduma.



Bi. Sultana Seiff
Meneja wa Usimamizi na Udhibiti wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao

# e-GA yasisitiza umuhimu wa nyaraka zinazotekelezeka katika usimamizi wa TEHAMA Serikalini

Na. Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Maafisa TEHAMA Serikalini, wametakiwa kuandaa nyaraka za usimamizi wa TEHAMA zinazotekelezeka ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa Serikali Mtandao kwenye taasisi zao.

Wito huo umetolewa na Meneja wa Huduma za Sheria wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi (SACP) Rafael Rutaihwa, wakati akifungua kikao kazi cha siku nne cha Maafisa TEHAMA wa Serikali, kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma. Kikao hicho, kililenga kuwajengea uwezo Maafisa hao katika uandaaji wa nyaraka mbalimbali za usimamizi wa TEHAMA zenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa Kanuni na Miongozo ya Serikali Mtandao.

Rutaihwa alisema kuwa, ukaguzi uliofanywa na e-GA umebaini uwepo wa nyaraka mbalimbali za usimamizi wa TEHAMA katika taasisi za umma, zisizotekelezeka kwa urahisi na hivyo kurudisha nyuma jitihada za Serikali Mtandao.

**"Tunahitaji kuboresha na kujua tunazitumiaje nyaraka hizi katika usimamizi wa TEHAMA kwenye taasisi zetu ili kufikia malengo ya kuwa na Serikali Mtandao yenye tija."**
SACP) Rafael Rutaihwa,
**Meneja Huduma za Sheria e-GA**

Aidha, alibainisha kuwa utengenezaji wa nyaraka zenye kukidhi Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, utasaidia kupunguza changamoto zinazojitokeza kutokana na ukosefu wa nyaraka sahihi za usimamizi wa TEHAMA, na hivyo kuwezesha utekekelezaji wa nyaraka hizo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali Mtandao.

"Ni muhimu kuhakikisha kuwa, nyaraka hizo zinaenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, ili kuongeza usalama, ufanisi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za kidijitali", alisisitiza Rutaihwa.

Kwa upande wake, Meneja wa Usimamizi na Udhibiti wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao Bi. Sultana Seiff, aliwataka wataalamu hao kuwa mfano wa kuigwa kwa taasisi nyingine kwa kuhakikisha kuwa kila taasisi inazo nyaraka zote tisa (9) muhimu zitakazotoa mwongozo katika usimamizi wa TEHAMA ndani ya taasisi.

Nyaraka hizo tisa (9) za usimamizi wa TEHAMA ni pamoja na Sera ya TEHAMA, Mpango Mkakati wa TEHAMA, Usanifishaji wa Mpango wa Shughuli, Sera ya Usalama wa TEHAMA, Sera ya Matumizi Rasmi ya TEHAMA, Mpango Mkakati wa Kujihami na Majanga ya TEHAMA, Taratibu za Usimamizi wa Huduma za TEHAMA, Taratibu za Usimamizi wa Miradi ya



Meneja wa Usimamizi na Udhibiti wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao Bi. Sultana Seiff akizungumza na washiriki wa kikao kazi cha uandaaji wa nyaraka mbalimbali za usimamizi wa TEHAMA

TEHAMA, na Taratibu za Ujengaji, Ununuzi, Uendeshaji na Usimamizi wa TEHAMA.

Alisema, ili kuwa na utekelezaji bora wa Serikali Mtandao wenye kuleta manufaa na tija katika utendaji kazi, ni vema wataalamu hao kufanya maboresho katika nyaraka hizo na kuhakikisha kuwa zinakwenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia.

**“Tufanye mapitio ya nyaraka zetu na kuhakikisha kuwa zinaenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na mazingira yetu ya kazi kwa ujumla.”**

Bi. Sultana Seiff,
**Meneja wa Usimamizi na Udhibiti wa Viwango na Miongozo.**

Akiongea kwa niaba ya washiriki wa kikao hicho, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA Bodi ya Sukari Tanzania Bw. Faustine Mgimba, aliipongeza e-GA kwa kuandaa kikao kazi hicho huku akieleza kuwa, ushirikiano wa karibu kati ya Mamlaka na wadau wake unaongeza umiliki wa nyaraka hizo na kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Kikao kazi hicho ni sehemu ya juhudi endelevu za e-GA katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA Serikalini, utoaji wa huduma bora, salama na zinazokidhi matarajio ya wananchi.



Mshiriki akisikiliza kwa makini mada zilizotolewa wakati wa kikao kazi cha uandaaji wa nyaraka mbalimbali za usimamizi wa TEHAMA

# Kutoka KILWA hadi SHENZHEN: Safari ya ndoto za kidijitali za Pulcheria




## Hadithi ya msichana aliyeshinda mashindano ya kitaifa ya TEHAMA, kusafiri hadi China, na sasa kutengeneza mifumo bunifu ya kidijitali serikalini

Na. Benchine Bago | Afisa Habari

Katika kitabu chake cha Lean It Mwanamama bilionea **Sheryl Sandberg** ametoa nukuu maarufu isemayo **'Fortune does favor the bold'**, kwa tafsiri rahisi ya Kiswahili ujumbe tunaoupata ni kwamba 'bahati huwadondokea wale walio na ujasiri au watu walio imara!

Kwa mujibu wa Bi. Sandberg, ambaye ndiye mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kuwa katika Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Meta inayomiliki mitandao ya kijamii ya Facebook, WhatsApp n.k, anaamini ujasiri ndio ngazi ya kwanza ya mafanikio.

Bi. Sandberg anaeleza kuwa, mafanikio hayaji kwa wale wanaokaa kimya au kusubiri mazingira yabadilike, bali kwa wale wanaothubutu kuchukua hatua. Jasiri hapa hakumaanishi mtu asiye na hofu, bali mtu anayekubali hofu lakini haruhusu hofu imtawale na kuizima ndoto yake, bali husonga mbele ili kupigania ndoto zake.

Anasisitiza kuwa, "bahati" mara nyingi inatokea kwa watu wanaojitokeza, wanaojaribu mambo mapya, na wanaoweza kuanguka kisha kusimama tena. Katika hatua ya kuanguka na kusimama tena, ndipo hupatika washindi na washindwa yaani **'winners and lossers'.** Washindi huinuka na kusimama tena na wanaoshindwa hukata tamaa baada ya kuanguka.

Bi. Pulcheria Sumia kutoka kitongoji cha Mnazi Mmoja wilaya ya Kilwa Masoko mkoani Lindi, yeye amechagua neno ushindi kuwa ndiyo ramani yake. Akiwa ni msichana mwenye umri wa miaka 23, anayetoka katika mazingira yasiyo na urafiki na TEHAMA, lakini kwa jitihada zake tayari jina lake limetambulika katika vitabu mbalimbali vya kumbukumbu ya maendeleo ya TEHAMA duniani.

Msichana huyu jasiri, alipata elimu yake ya msingi katika Shule ya msingi Ukombozi iliyopo Kilwa Masoko, na kisha akajiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ilulu iliyopo Kilwa Njia Nne, na baadaye akajiunga na Shule ya Sekondari ya Juu 'Mahiwa High School' ambayo nayo inapatikana katika kata ya Nyangao, halmashauri ya Mtama, mkoani Lindi.

Baada ya kuhitimu safari ya elimu ya Sekondari, Bi.

Pulcheria alijiunga na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kusomea Shahada ya Awali ya Sayansi katika Mifumo ya Habari za Afya.

Mwaka 2023, akiwa mwaka wa pili katika chuo hicho ndipo 'nyota ya jaha' ilionekana kwake, milango ilianza kufunguka na kumuonesha picha ya matumiani katika kufikia ndoto yake yakuwa mbobezi wa TEHAMA'.

Nyota ya Pulcheria ilianza kung'ara baada ya kushiriki na kushinda Mashindano ya Kitaifa ya TEHAMA yaliyoandaliwa na Kampuni ya Huawei (Huawei ICT competition) akishindana kwenye kipengele cha 'cloud track'

**"Niliposikia fursa ya kushiriki mashindano haya niliona hii ndiyo njia pekee ya mimi kuonesha uwezo wangu. Lakini kitu pekee kilichokuwa kinanipa mawazo ni hofu, katika mazingira niliyotoka ni nadra sana kuona mtoto wa kike anaenda kushindana na wanaume, lakini nilijipa moyo."**

Bi. Pulcheria Sumia
**Mtaalamu wa TEHAMA**

Baada ya kukamilisha hatua zote za ushiriki, Pulcheria aliibuka kuwa miongoni mwa washindi watatu (3), kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, huku yeye akiwa msichana pekee katika kundi hilo la washindi na hivyo kupata nafasi ya kuwakilisha Tanzania, katika hatua ya Afrika ambako hakufanikiwa kusonga mbele.

"Kuwa miongoni mwa wawikilishi wa Tanzania katika mashindano haya ilikuwa ni hatua kubwa ya kujifunza na kusonga mbele, faida kubwa niliyoipata ni ile nguvu na matamanio ya kuvuka hatua ya Afrika na kwenda kushindana kwenye jukwaa la dunia nzima," alieleza Bi. Pucheria.

Kwa vile ndoto yake kubwa ni kuhakikisha anaingia ubia na TEHAMA ili asaidie kutatua changamoto za jamii yake, msichana huyu ameamua kupambana na kuvuka vikwazo vya njiani ili kufika pale anapopaamini.

Mnamo Novemba 2024, Bi. Pulcheria alifanikiwa kupata nafasi ya kushiriki kwenye warsha ya 'Huawei Seeds for the Future' akiwa kati ya vijana 10, miongoni mwa mamia waliofanya mtihani wa kujiunga na programu hiyo kutoka vyuo mbalimbali vinavyofundisha masomo ya TEHAMA kusini mwa jangwa la Sahara.

"Ilikuwa furaha sana kwangu, maana kabla ya kuja Dodoma sijawahi kutoka nje ya mikoa ya Pwani, nimeishi Kilwa Masoko (Lindi) na Kibiti (Pwani), hivyo fursa hii kwangu ilikuwa ni alama muhimu katika maisha yangu." alieleza Pulcheria.
Kupitia warsha hii iliyofanyika katika mji wa Shenzhen, Pulcheria anasema alipata nafasi ya kujifunza teknolojia bunifu, kuunganishwa na wataalamu wa sekta ya TEHAMA duniani, na kujipatia maarifa mapya yatakayomsaidia kuchangia kwenye maendeleo ya kidijitali nchini Tanzania.

"Warsha ya Seeds for the Future ilinifungua macho. Nimejifunza mengi kuhusu miradi ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence - AI), ambayo tayari China imefanikiwa kuitekeleza, mfano mfumo wa kurejesha umeme kiotomatiki unaoendeshwa na akili bandia (AI). Niliona kuwa, teknolojia hiyo ingeweza kufaa sana katika jamii zetu ambako tatizo la kukatika kwa umeme ni la mara kwa mara." aliefafanua.

Pulcheria anasema, katika safari hii ya Uchina katika mji wa Shenzhen ambao ndiyo kitovu cha TEHAMA nchini humo, ilimpa fursa ya kukutana na vijana mbalimbali kutoka pembe zote za dunia, kubadilishana mawazo na kuongeza mtandao wa marafiki, anaondelea kushirikiana nao katika masuala ya TEHAMA.

Kwa sasa Pulcheria ni mwajiriwa katika Ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, jijini Dodoma.

Pulcheria anaamini kuwa, uwepo wake katika kituo hicho ni sehemu ya kujijenga na kujiimalisha zaidi katika kutimiza ndoto zake katika sekta ya TEHAMA.

Hadi sasa akiwa e-GA, ameshashiriki katika usanifu wa mifumo mbalimbali ikiwemo 'MsaadaAI' na mfumo wa Kuchambua Hisia (sentiment analysis) ambayo miradi hii bado inaendelea kufanyiwa kazi katika kituo hicho.

Hadithi ya Pulcheria Sumia ni ushahidi kuwa bidii, uthubutu, na kujiamini vinavyoweza kufungua milango ya mafanikio. Safari yake kutoka Kilwa Masoko hadi Uchina, inatoa taswira ya wazi kwamba nguvu uliyonayo, nia na dhamira ya dhati inaweza kuwasha moto wa mafanikio, na joto lake likakupa faraja wakati wa baridi kali ikiwa ni sehemu ya mapito katika safari ndefu ya maisha.



Dkt. Isaac Rugemalila
Daktari Bingwa Mbobezi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa

# Asilimia kubwa ya Wafanyakazi Wanakabiliwa na Matatizo yanayohusiana na Afya ya akili

Na. Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Katika ulimwengu wa kazi wa sasa, afya ya akili ni moja ya changamoto kubwa inayopuuzwa kwa muda mrefu. Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia kubwa ya wafanyakazi wanakabiliwa na matatizo yanayohusiana na afya ya akili, huku asilimia 15 tayari wakibainika kuwa na magonjwa ya akili. Hali hii inaashiria tatizo kubwa linalohitaji uangalizi wa haraka kutoka kwa waajiri, Serikali na jamii kwa ujumla.

Mazingira ya kazi yamekuwa na msukumo mkubwa unaochangia kuibuka kwa matatizo ya akili. Shinikizo la kazi, malengo magumu kufikiwa, ukosefu wa usalama wa ajira, pamoja na saa ndefu za kazi, vimechangia kwa kiasi kikubwa kuathiri afya ya akili ya wafanyakazi.

Wafanyakazi wengi hujikuta wakiwa na msongo wa mawazo, wasiwasi, au mfadhaiko bila hata wao wenyewe kutambua hali walizonazo. Hii ndiyo sababu inayochangia idadi kubwa ya wafanyakazi kuwa katika hatari ya magonjwa ya akili.

Daktari Bingwa Mbobezi wa Afya na Magonjwa ya Akili (Matibabu ya Watu Walioathirika na Pombe na Dawa za Kulevya) Dkt. Isaac Rugemalila kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, anasema kuwa unyanyapaa uliopo kuhusu magonjwa ya akili bado ni kikwazo kikubwa katika maeneo ya kazi, hali inayofanya wafanyakazi wengi kuogopa kujitokeza na kueleza changamoto zao za kiakili kwa hofu ya kubaguliwa au kuonekana dhaifu.

Athari za hali hii haziwaathiri wafanyakazi pekee bali pia waajiri na uchumi kwa ujumla. Wafanyakazi wenye matatizo ya akili hupunguza ufanisi kazini, huongeza utoro au migogoro kazini. Gharama za matibabu na upotevu wa uzalishaji huongezeka, hali inayodhoofisha maendeleo ya taasisi na taifa kwa ujumla.

## Lakini Magonjwa ya afya ya akili ni nini?

Ni hali au matatizo yanayoathiri uwezo wa kufikiria, hisia, tabia na kutenda na hivyo kumpelekea mtu kushindwa kutambua changamoto za kila siku za maisha. Magonjwa haya si dalili ya udhaifu, bali ni matatizo ya kiafya kama magonjwa mengine.

- Dkt. Rugemalila anasema kuna aina za magonjwa ya afya ya akili takribani 297. Magonjwa haya yanaweza kuathiri mtu yeyote—mtoto, kijana au mtu mzima. Ingawa magonjwa mengi yamekuwa yakionekana kati ya umri wa miaka 10-35.
- Kulingana na tafiti zilizofanyika, Dkt. Rugemalila anasema mtu mmoja kati ya watu

wanne ana changamoto ya afya ya akili, huku watu millioni 7 duniani wakiwa na dalili za magonjwa ya afya ya akili.

- Sababu zipi hupelekea Magonjwa ya Afya ya akili?
- **Kibailojia (Vinasaba):** Asilimia 40-60 ya magonjwa ya akili hutokana na kurithi kutoka kwa wazazi. Mtu hurithi udhaifu wa kemikali za ubongo. Baadhi ya magonjwa ya akili kama schizophrenia, bipolar, sonona huweza kurithiwa.
- **Umri:** Mabadiliko ya umri huathiri mwili na akili. Ikumbukwe kuwa ubongo hubadilika kulingana na umri. Baadhi ya magonjwa ya akili huonekana katika umri fulani zaidi au mtu anayeweza kuyapata kutokana na umri wake.
  - Vijana wanaweza kupata magonjwa ya akili kutokana na mabadiliko ya homoni ambayo husababisha msukumo wa hisia
  - **Wazee:** kudhoofika kwa kumbukumbu na ubongo.
- **Uzito mkubwa:** huathiri afya ya mwili na akili. Kutozingatia mlo kamili hupelekea kuwa na uzito mkubwa kupita kiasi.
- **Kuwa na maradhi ya magonjwa sugu (figo, moyo, ini)**: Magonjwa haya ya muda mrefu huathiri maisha kwa ujumla, huleta hofu ya kifo. Matumizi ya dawa kwa muda mrefu huathiri ubongo.
- **Jinsia:** Baadhi ya magonjwa ya afya ya akili yanaathiri jinsia ya kike zaidi kuliko ya kiume hii inatokana na kwamba, mwanawake anapoingia katika siku zake (hedhi) kuna 'hormones' ambazo hutolewa kipindi hicho.
- **Msongo wa maisha** (umasikini, kukosa ajira, matatizo ya kifamilia) Huharibu usingizi na kumbukumbu na kusababisha msongo wa mawazo.
- **Matumizi ya dawa za kulevya** (pombe, bangi, cocaine, heroin) huathiri zaidi wanawake kwani kutokana na maumbile. Mwanamke anahifadhi kubwa ya mafuta mwili mwake hivyo dawa za kulevya hujihifadhi kwenye mafuta hayo.

## Dalili za Magonjwa ya Afya ya Akili.

Changamoto hii inaweza kudhibitiwa endapo dalili za matatizo ya akili zitatambuliwa mapema na hatua sahihi zitachukuliwa mapema. Wafanyakazi wenye changamoto ya afya akili huonyesha dalili zifuatazo;

- Kupungua uwezo wa kufikiria, kuhisi, kutenda au vyote kwa pamoja.
- Kutozingatia usafi binafsi
- Mahusiano na watu yanapungua
- Kupungua kwa uwezo wa kufanya kazi
- Matibabu ya Magonjwa ya Afya ya Akili
- Dkt. Rugemalila anasema matibabu ya Afya ya Akili yamegawanyika katika sehemu kuu mbili;
- Tiba ya Kisaikolojia (Psychotherapy / Counselling), hii ni tiba ya mazungumzo kati ya mtaalamu na mgonjwa.
- Matibabu kwa kutumia dawa.

## Matibabu haya yanatolewa kwa kuzingatia;

- Aina ya ugonjwa wa akili,
- Ukali wa ugonjwa,
- Umri na hali ya mgonjwa,
- Uwepo wa magonjwa mengine ya mwili.
- Kinga ni Bora kuliko Tiba

Dkt. Rugemalila anashauri waajiri kuwekeza katika programu za afya ya akili mahali pa kazi, ikiwemo ushauri nasaha, mafunzo ya kudhibiti msongo wa mawazo, na kuunda mazingira rafiki yanayohimiza mawasiliano ya wazi. Vilevile, sera zinazolinda haki na ustawi wa wafanyakazi zinapaswa kuimarishwa ili kupunguza shinikizo lisilo la lazima.

Anasema, elimu sahihi kuhusu magonjwa ya akili ni muhimu ili kuondoa unyanyapaa uliopo. Elimu hii itawasaidia wafanyakazi kutambua dalili mapema na kutafuta msaada kabla hali haijawa mbaya zaidi.

"Waajiri waongeze uwezo kwa wafanyakazi kuweza kupambana na changamoto za maisha, hii itawasaidia wafanyakazi kudhibiti msongo wa mawazo," alisisitiza Dkt. Rugemalila.

Dkt. Rugemalila alitoa wito kwa watumishi kuweka kipaumbele katika afya ya akili kwa kutenga muda wa kutosha wa kupumzika kati ya masaa 6 hadi 8 na kufanya mazoezi.

Anamaliza kwa kusema kuwa **"Maadamu una ubongo, upo katika hatari ya kupata ugonjwa wa afya ya akili"** Tafuta mapema huduma ya afya ya akili ili kujenga nguvu kazi yenye afya, tija na ustawi endelevu.



## Mapinduzi ya Serikali Mtandao - Halmashauri ya Wilaya ya Geita

# Mapato yaongezeka kutoka Bilioni 4 hadi Bilioni 18 kwa Mwaka

Na. Benchine Bago | Afisa Habari

Halmashauri ya Wilaya ya Geita ni miongoni mwa mifano halisi ya namna Serikali za Mitaa zinavyoweza kubadili mfumo wa utendaji kupitia matumizi shirikishi ya TEHAMA sambamba na kuongeza mapato.

Matumizi bora ya TEHAMA yaliiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Geita, kutunukiwa tuzo na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ya Halmashauri zinazofanya vizuri katika utekelezaji wa viwango na miongozo ya Serikali Mtandao mwaka 2024.

Tuzo hizo zilizotolewa katika Kikao kazi cha Nne cha Serikali Mtandao jijini Arusha, ziliifanya halmashauri hiyo kuwa mshindi wa jumla na pekee katika kundi la halmashauri nchini.

Mageuzi haya hayakutokea kwa bahati, bali yametokana na uwekezaji, maono na usimamizi makini wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika shughuli za kila siku za utendaji kazi wa halmashauri hiyo, na hivyo kuleta matokeo chanya katika maeneo mbalimbali ikiwemo mapato.

**“Mifumo imetufungua macho. Kile tulichokuwa tunaamini kuwa hakiwezekani miaka ya nyuma, leo tunakifanya kwa ufanisi, kwa uwazi na kwa gharama nafuu zaidi.”**

Dkt. Alphonce Bagambabyaki.
**Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita.**

Anaeleza kuwa, awali Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilikuwa ikikusanya takribani Shilingi Bilioni 4 hadi 5 kwa mwaka. Utaratibu wa ukusanyaji wa mapato ulikuwa wa analojia uliohusisha makisio ya makadiriro ya kodi, njia hii ilisababisha urasimu na upotevu mkubwa wa mapato kutokana na ukosefu wa taarifa sahihi.

Baada ya kuanzisha na kuimarisha matumizi ya Serikali Mtandao kupitia mifumo ya ukusanyaji mapato ukiwemo Mfumo wa TAUSI, imechangia kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato katika halmashauri hiyo.

Katika kipindi cha hivi karibuni, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imefanikiwa kukusanya hadi Shilingi Bilioni 10, kiwango kilichovuka hata bajeti ya mwaka ya halmashauri ya Shilingi Bilioni 8.7.

"Kwa mara ya kwanza, tuliona mapato yetu yanazidi bajeti tuliyojiwekea tulizalisha ziada ya takribani bilioni 1.7. Huu ulikuwa uthibitisho wa moja kwa moja kwamba mifumo ya TEHAMA ina tija isiyopingika", anafafanua Dkt. Bagambabyaki.

Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, halmashauri hiyo inalenga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 18 sawa na mara tatu ya kiasi kilichokuwa kikikusanywa kabla ya kuanza kutumia mifumo ya TEHAMA.

Mafanikio haya kwa kawaida yangetumia miaka mingi kufikiwa kwa utaratibu wa awali wa makusanyo katika Serikali za Mitaa, lakini matumizi ya Serikali Mtandao yamewezesha mafanikio haya kwa muda mfupi kwa kuongeza uwazi, udhibiti na ufuatiliaji wa vyanzo vya mapato.

Kwa kutambua na kutumia nadharia ya Mtiririko wa Fedha (Cash Flow Theory ya John Burr Williams), Halmashauri ya Wilaya ya Geita iligundua ustawi wake hutegemea uwezo wake wa kudhibiti mtiririko wa fedha, hivyo ikahakikisha mapato yanaongezeka kuliko matumizi, ili halmashauri iweze kukua, kujiendesha, kulipa madeni, na kupanua huduma bora kwa wananchi.

Baada ya kuimarisha mapato, halmashauri ilijiwekea lengo la kuwa na Mifumo ya Serikali Mtandao inayowezesha kupunguza matumizi ya fedha katika utendaji kazi wa kila siku wa halamshauri.

Kabla ya mageuzi ya Serikali Mtandao, Halmashauri Wilaya ya Geita ilitumia kiasi kikubwa cha fedha kununua vifaa mbalimbali vya kiofisi 'stationaries', hususan karatasi, majalada, wino kwa ajili mashine za kurudufu n.k. Kwa mujibu wa Dkt. Bagambabyaki, kila mwaka halmashauri ilitumia kati ya shilingi milioni 150 hadi milioni 200 kwa matumizi ya karatasi pekee.

Aidha, kupungua kwa matumizi ya karatasi kumeongeza uwazi, uwajibikaji na utunzaji wa taarifa katika halmsahauri, huku urasimu ukipungua kwa kiwango kikubwa.

"Hakuna majalada makubwa yenye kusheheni karatasi, hakuna makabati yaliyosheheni nyaraka, na hakuna stakabadhi zinazopotea kwa urahisi kwa sababu kila huduma inaanzia na kukamilika kwenye mifumo kupitia mfumo wa ofisi mtandao (e-Office)" anasisitiza Dkt. Bagambabyaki

Vilevile katika uendeshaji wa Baraza la Madiwani la hamashauri, linatumia Mfumo wa Kidijiti wa Uendeshaji wa Vikao wa e-Board, hivyo ufanisi umeongezeka, na kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao vya baraza hilo.

Kwa upande mwingine, uwepo wa mifumo ya TEHAMA umerahisishia utendaji kazi kwa watumishi wa halmashauri ambao vituo vyao vya kazi vipo mbali na ofisi za halmashauri. Matumizi ya mfumo wa utendaji wa watumishi wa e-watumishi, unaiwezesha halmashauri kushughulikia masuala ya kiutumishi kwa wakati hata kwa wale walio mbali na halmashauri.

Dkt. Bagambabyaki anaeleza kuwa, kabla ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA, watumishi kutoka maeneo ya mbali kama vile Butundwe, Nyakagwe au Izumacheli walilazimika kusafiri kwa zaidi ya saa 5 hadi 7 kwenda wilayani (Nzera) kuwasilisha taarifa za kiutumishi, kusainiwa barua au stakabadhi.

**"Safari hizi zilihitaji muda, mafuta, posho, na wakati mwingine zilichelewesha ushughulikiaji wa masuala ya kiutumishi na utoaji wa huduma kwa wananchi katika maeneo husika."**

Anabainisha kuwa, halmashauri ilifanya tathmini na kubaini kuwa, ilikuwa ikitumia kati ya Shilingi milioni 50 hadi 60 kila mwaka kwa ajili ya gharama za kusafiri na usafirishaji wa watumishi na nyaraka. Kwa sasa taarifa zinatumwa kidijitali, barua zinasainiwa kidijitali, wakati wowote na hivyo kupunguza gharama na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**"Leo hii hakuna tena sababu ya mtu kusafiri kwa muda mrefu kuleta karatasi, Mifumo imerahisisha kila kitu tumeokoa muda, tumepunguza gharama na tumeongeza ufanisi wa utoaji huduma"**,

Kwa sasa halmashauri ya wilaya ya Geita imeweza, kujenga madarasa zaidi kuliko miaka ya nyuma, kuimarisha miundombinu na huduma katika Vituo vya Afya na Zahanati, kupanua miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo maji na barabara pamoja na kuimarisha miradi ya maendeleo inayogusa wananchi moja kwa moja.

Mafanikio haya yanatokana na kuongezeka kwa mapato halisi, kupunguza upotevu wa rasilimali na kuongeza kasi ya utendaji.

"Leo tuna fedha za kutekeleza miradi ambayo zamani ilikuwa changamoto. TEHAMA haijaongeza mzigo, imeongeza uwezo. Huu ni ushahidi kwamba ukitumia mifumo sahihi, unabadilisha maisha ya watu." anasisitiza Dkt. Bagambabyaki

Mafanikio ya halmashauri hii yanaonesha wazi kwamba matumizi sahihi ya Serikali Mtandao hayapaswi kuonekana kama kikwazo katika maendeleo, bali ni uwekezaji unaoleta tija kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Kwa halmashauri ya wilaya ya Geita, mageuzi haya ni mwanzo tu. Kama anavyosema Dkt. Bagambabyaki, "Bado tuna safari ndefu, lakini msingi tumeuweka" na msingi huo ni Serikali Mtandao yaani matumizi ya TEHAMA katika shughuli zote za Serikali.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Dkt. Alphonce Bagambabyaki



'Mifumo ya utoaji wa huduma za Serikali kidijitali imetusaidia kupata huduma kwa haraka, mfano huduma ya kulipia umeme kwa njia ya simu huokoa muda na gharama, zamani tulilazimika kufika katika vituo vya kutolea huduma na kupanga foleni kwakuwa vilikuwa vichache, lakini kwa sasa tunaweza kulipia umeme na huduma nyinginezo tukiwa nyumbani, tena kwa muda mfupi kabisa tunapata umeme''

**Noela Nicholaus**
Mkazi wa kitunda Dar es Salaam.



''Teknolojia ni kiwezeshi na kama nchi tunazidi kuendelea , teknolojia imeboresha maisha yetu kwa sasa kila kitu kinafanyika kupitia mifumo, tunafanya malipo kwa control namba ambazo zinatolewa na Serikali jambo linalotufanya tuamini kile tunacholipia kinaenda Serikalini moja kwa moja, tofauti na ilivyokuwa awali tulipokuwa tunalipa kwa watu mikononi tulikuwa hatuamini kama zinafika sehemu husika"

**Godwin Ngwilimi**
Mkazi wa Mbezi Dar es Salaam.



"Hapo mwanzo kabla ya hii mifumo, shughuli nyingi zilikuwa zinatumia mchakato mrefu sana, yaani kupata huduma fulani ilikuwa ni lazima utumie muda mrefu au gharama kubwa, lakini kwa sasa ujio wa mifumo umerahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa jamii kwa haraka na kwa wepesi, tunaiomba Serikali iboreshe mifumo hii ili iweze kupatikana muda wote'

**Joshua Antony**
Mkazi wa Ilala Dar es Salaam.



''Moja ya faida kubwa ya hii mifumo ya Serikali ni kuwa inaturahisishia wananchi kupata huduma kwa haraka na kuepuka gharama mbalimbali ambazo tungekutana nazo kama mifumo hii isingekuwepo, kwa sasa karibu huduma zote zinapatikana kwenye simu, na pia tumekuwa tukipokea taarifa mbalimbali za Serikali kwa njia ya ujumbe mfupi kupitia simu zetu za kiganjani, jambo ambalo kwakweli limetufanya kupata taarifa sahihi na kwa wakati'

**John Kimaro**
Dar es Salaam.

# Tuzo



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji Zanzibar Mhe. Khamis Suleiman Mwalimu akimkabidhi tuzo ya Ubunifu wa TEHAMA katika Sekta ya Umma na Uunganishaji wa Mifumo kwa mwaka 2025 katika kipengele cha tuzo ya Serikali Mtandao, Mkurugenzi wa Miundombinu na Uendeshaji (e-Ga) Bw. Benjamin Dotto kwenye tuzo za Utumishi wa Umma na Ubunifu Tanzania (TPSIA 2025).



Wadau mbalimbali waliopokea tuzo, wakiwa katika picha ya pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji Zanzibar Mhe. Khamis Suleiman Mwalimu (Aliyesimama katikati) kwenye tuzo za Utumishi wa Umma na Ubunifu Tanzania (TPSIA 2025).

# Maonesho



Waziri wa Uchukuzi Prof Makame Mbarawa akizungumza na Afisa Habari mwandamizi wa e-GA Bi. Catherine Peter wakati alipotembelea banda la maonesho la e-GA wakati wa maonesho ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar Es Salaam





Afisa Habari mwandamizi wa e-GA, Bi. Catherine Peter akitoa Elimu ya Huduma za Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa mdau wa Serikali Mtandao alipotembelea banda la maonesho la e-GA wakati wa maonesho ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar Es Salaam

# Mafunzo



Watumishi mbalimbali kutoka sekta ya Afya wakiwa kwenye mafunzo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Tovuti za Serikali, kwa Wakuu wa Vitengo vya Habari na Mawasiliano Serikalini, pamoja na Maafisa Habari wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya yaliyofanyika Mjini Morogoro



Washiriki kutoka Taassi mbalimbali za Umma wakiwa katika kikao kazi cha kuwajengea uwezo katika uandaaji wa nyaraka mbalimbali za usimamizi wa TEHAMA kilichofanyika jijini Dodoma

**Ili kupata Huduma za Serikali Kiganjani mwako**




Ofisi ya Rais,
Mamlaka ya Serikali Mtandao,
Mtumba-Mtaa wa Mawasiliano,
S.L.P 2833, 40404 DODOMA.
Barua pepe: barua@ega.go.tz
Simu: +255 026 - 296 1957

Karibu tujijenge Serikali Kidijitali